**Nambari ya Mtahiniwa ________________**

**SMZ**

**BARAZA LA MITIHANI LA ZANZIBAR**

**MTIHANI WA KUINGILIA KIDATO CHA KWANZA**

**126** **HISTORIA**

**MUDA: SAA 2.00** **JUMATATU 02 DISEMBA, 2019 ASUBUHI**

**MAELEKEZO KWA WATAHINIWA**

1. **Mtihani huu una sehemu TATU (3) A, B na C.**
2. **Jibu maswali YOTE kutoka sehemu A na B. Jibu maswali MANNE (4) kutoka sehemu C.**
3. **Andika nambari yako ya mtihani katika kila ukurasa.**
4. **Majibu yote yaandikwe katika nafasi zilizowekwa.**
5. **Majibu yote yaandikwe kwa kalamu ya buluu au nyeusi.**
6. **Simu za mkononi haziruhusiwi ndani ya chumba cha mtihani.**

| KWA MATUMIZI YA WASAHIHISHAJI | | |
|---|---|---|
| NAMBARI YA SWALI | ALAMA | SAINI |
| 1. | | |
| 2. | | |
| 3. | | |
| 4. | | |
| 5. | | |
| 6. | | |
| 7. | | |
| 8. | | |
| 9. | | |
| 10. | | |
| 11. | | |
| JUMLA | | |

**Mtihani huu una kurasa 8 zenye maandishi**

**Nambari ya Mtahiniwa ________________**

## SEHEMU A: (Alama 20)

**Jibu maswali YOTE katika sehemu hii.**

1. Chagua jawabu sahihi na uandike herufi yake katika jadweli lililopo hapo chini.

i. Elimu bora zaidi wakati wa ukoloni walipatiwa

A. Watoto wa Kiafrika B. Watoto wa Kizungu

C. Watoto wa Machifu D. Watoto wa Kiasia

ii. Nchi iliyopata uhuru kwa njia ya mazungumzo tu katika bara la Afrika ni

A. Tanganyika B. Msumbiji

C. Ghana D. Zimbabwe

iii. Utaalamu wa kupata chuma kutoka kwenye udongo au mawe ulifanyika kwa

A. Kufinyanga chuma na udongo

B. Kuyeyusha mawe na udongo kwa moto

C. Kuyeyusha chuma halisi na mawe kwa moto

D. Kufinyanga mawe na udongo

iv. Jamii za Watanganyika zilizoishi maisha ya ujima ni

A. Wandorobo na Wahadimu B. Wasandawe na Wahadimu

C. Wahadimu na Wahadzabe D. Wasandawe na Wahadzabe

v. Vita vya kwanza vya dunia vilipiganwa mwaka

A. 1905 - 1907 B. 1910 - 1912

C. 1914 - 1918 D. 1918 – 1919

vi. Mkutano wa Berlin ulishirikisha mataifa ya Ulaya

A. Kumi na tatu B. Kumi na nne

C. Kumi na tano D. Kumi na sita

vii. Miongoni mwa athari za wageni kutoka Ulaya kwa nchi za Kiafrika ni

A. Kuibuka kwa dini ya Majusi B. Kuibuka kwa dini ya Budha

C. Kuibuka kwa dini ya Kikristo D. Kuibuka kwa dini ya Kiislamu

viii. Pepo za kaskazi zilivuma kutoka kaskazini kuelekea

A. Kaskazini mashariki
B. Kaskazini magharibi
C. Kusini magharibi
D. Kusini mashariki

ix. Kabla ya Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964, mashamba ya mikarafuu na minazi yalinunuliwa na

A. Waarabu
B. Wahindi
C. Wachina
D. Waingereza

x. Mfumo wa biashara wa kuleta bidhaa kutoka Ulaya ulihamasisha

A. Ukuaji wa biashara ndogo ndogo
B. Ukuaji wa kilimo
C. Ukuaji wa viwanda vya mkoloni
D. Ukuaji wa ufugaji

**JAWABU**

| i. | ii. | iii. | iv. | v. | vi. | vii. | viii. | ix. | x. |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | | |

2. Andika **Kweli** mbele ya maelezo sahihi au **Sikweli** mbele ya maelezo yasiyo sahihi.

i. Vyama vingi vya siasa nchini Zimbabwe vilipigwa marufuku na Serikali ya Kikoloni. ________

ii. Waingereza na Sultani hawakushirikiana kutawala Zanzibar. ________

iii. Wakati wa ukoloni Waafrika walipewa ardhi yenye rutuba kwa ajili ya kilimo. ________

iv. German East Africa Company iliongozwa na Bw. Karl Peters. ________

v. Bidhaa za pembe za ndovu na dhahabu zilieverywhere letwa na wageni kutoka Bara la Asia. ________

vi. Samora Machel alikuwa mfanyabiashara aliyefika Afrika. ________

vii. Kuoana, kuzaliana na kuhamahama ni sababu za kuenea kwa utaalamu wa chuma Afrika Mashariki. ________

viii. Hemed bin Mohamed (Tippu Tipu) alifanya biashara ya madini. ________

ix. Wageni kutoka Ulaya walisaidia kukua kwa lugha ya Kiswahili katika pwani ya Afrika ya Mashariki. ________

x. Elimu bure ni moja kati ya Matunda ya Muungano wa Zanzibar na Tanganyika. ________

Nambari ya Mtahiniwa ________________

**SEHEMU B: (Alama 40)**

**Jibu maswali YOTE katika sehemu hii**

3. Linganisha miaka kutoka **KIFUNGU A** na matukio muhimu kutoka **KIFUNGU B.** Andika herufi ya jawabu ndani ya jadweli liliopo hapo chini.

| KIFUNGU A | KIFUNGU B |
|---|---|
| i. 1938 | a. Kifo cha Mwalimu J. K. Nyerere |
| ii. 1961 | b. Kurejeshwa kwa mfumo wa vyama vingi vya siasa nchini Tanzania |
| iii. 1964 | c. Uhuru wa Zimbabwe |
| iv. 1980 | d. Vita vya Majimaji |
| v. 1992 | e. Basukuma Union |
| | f. Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar |
| | g. Mwisho wa biashara ya utumwa Zanzibar |
| | h. Uhuru wa Tanganyika |

**JAWABU**

| i. | ii. | iii. | iv. | v. |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |

4. Jaza nafasi zilizo wazi kwa kuchagua jibu sahihi kutoka kwenye mabano yaliyopo hapo chini.

a) Msikiti wa Kizimkazi ulikuwa wa mwanzo kujengwa ________________________________ mwa kisiwa cha Unguja.

b) Viwanja vya michezo vya _______________________ Unguja na ______________________ Pemba vilijengwa baada ya Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964.

c) Kundi la mwanzo lililokuja Afrika kutoka Ulaya ni __________________________________.

d) Magofu ya Kaole yapo __________________________________ nchini Tanzania.

e) Mkuu wa mji au mtaa aliyekubaliwa na watu alikuwa akiitwa ________________________.

**(Gombani, Kaskazini, Wapelelezi, Bagamoyo, Amani, Jumbe, Wamishionari, Kusini)**

5. Jibu maswali yafuatayo kwa ufupi.

a) Taja sehemu mbili (2) ambazo walipelekwa watumwa walionunuliwa Afrika.

i) ______________________ ii) ______________________

b) Toa tofauti moja (1) tu kati ya Ukoloni na Ubepari.

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

c) Orodhesha makabila mawili (2) ya Tanganyika yaliyoungana na Wajerumani kupambana dhidi ya Wahehe.

i) ______________________ ii) ______________________

d) Ainisha sifa mbili (2) za msingi alizotakiwa kuwa nazo Mtanganyika katika Uchaguzi Mkuu wa Agosti 1960.

i) ______________________________________________

______________________________________________

ii) ______________________________________________

______________________________________________

e) Andika urefu wa istilahi zifuatazo.

i) ZRB ______________________________________________

______________________________________________

ii) TAZARA ______________________________________________

______________________________________________

**Nambari ya Mtahiniwa ________________**

**SEHEMU C: (Alama 40)**

**Jibu maswali MANNE (4) tu katika sehemu hii**

6. Orodhesha madhumuni manne (4) ya harakati za awali za kudai uhuru Tanganyika.

7. Elezea kwa ufupi faida nne (4) za matumizi ya zana za chuma wakati wa zama za chuma.

8. Ainisha mabadiliko manne (4) yaliyojitokeza katika sekta ya afya barani Afrika baada ya kupata uhuru.

9. Bainisha athari chanya tano (5) za kuingia kwa wageni Zanzibar kutoka Asia.

10. Andika maelekezo manne (4) aliyoyapokea Gavana kutoka Serikali ya Kikoloni.

11. Eleza makubaliano manne (4) yaliyofikiwa na mataifa ya kibeberu baada ya Mkutano wa Berlin wa mwaka 1884 -1885.

===================